



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**



**Taarifa namba: 056**

**10/01/2023**

**TAARIFA KWA UMMA**

**TAARIFA KUHUSU CHOO KILICHOFUNGWA CHA SOKO KUU TUNDUMA**

Kumekuwa na taarifa zikirushwa katika mitandao ya kijamii zikisema **Halmashauri ya Mji Tunduma imefunga choo cha soko kuu la Tunduma kwa muda wa miezi mitatu na kufanya wafanyabiashara kuteseka, na baadhi yao kuomba choo kirudishwe kwa mzabuni wa aliyekuwa akikiendesha hapo awali.**

Halmashauri inakanusha taarifa hiyo kwani choo hicho kilifungwa kwa muda wa miezi miwili tu na sasa kimeanza kufanya kazi tangu tarehe 09/01/2023.

Sababu kuu ya kufungwa choo hicho ni matengenezo makubwa yaliyoambatana na kubadilisha mfumo wa mashimo ya maji taka kutoka mfumo wa zamani wa Shimo moja na kutengeneza mfumo wa kisasa wa (biodigester system) ambao hauhitaji kunyonya maji taka na choo hakiwezi kujaa tena.

Baada ya kuona choo hiki kikijaa kila baada ya wiki mbili na kusababisha kutiririsha maji na kuhatarisha afya, Halmashauri ilikaa kikao na uongozi wa Soko pamoja na wafanyabiashara wote wa soko na kukubaliana kukifunga ili kifanyiwe matengenezo hayo ya muda mfupi.

Baada ya maridhiano kwa pande zote wafanyabiashara walikubaliana kutumia vyoo katika masoko jirani kama vile soko la Manzese lenye vyoo 03, soko la kisimani karibu na msikiti lenye vyoo 02 na Afrikana lenye vyoo 2 wakati choo cha soko hilo kikiwa katika matengenezo.

Ikumbukwe choo hiki tangu kimetengenezwa mwaka 2012 kilikuwa hakijawahi kufanyiwa matengenezo makubwa kwani kilikuwa kinaendeshwa na mzabuni ambaye alikuwa analipa 300,000/= kwa mwezi.

Kutokana na mkataba wa mzabuni kuisha Halmashauri ilikichukua choo hiki tangu mwezi Oktoba 2021 na tangu hapo mapato ya choo hicho yalipanda toka Tsh. 300,000/= alizokuwa anatoa Mzabuni kwa mwezi hadi kufikia Tsh. 3,000,000/= kwa mwezi. **Hapo wastani mzabuni alikuwa analipa ELFU KUMI KWA SIKU wakati Halmashauri ilipoanza kukusanya yenyewe mapato yakawa LAKI MOJA KWA SIKU**

Uamuzi wa kubadilisha mfumo wa majitaka katika choo hiki ni kutokana na gharama za kunyonya maji machafu ambazo kila mwezi ilitumika Tsh. 4,000,000/= kwa sasa tatizo hilo halita kuwepo tena na choo kimeanza kutumika na hakina changamoto yoyote.

Hata hivyo waraka wa serikali namba 16 wa 2016 ulitoa maelekezo kwa kuzitaka Mamlaka za Serikali za mitaa kukusanya mapato zenyewe kwa vyanzo wanavyoweza kuvikusanya ili kuongeza mapato ya serikali lengo kuu ni kukuza mapato ya Halmashauri. Kwa hali hiyo Halmashauri ya Mji Tunduma haitoweza kumrudishia chanzo hicho wakala wa awali kwani **mapato yake yameongezeka mara kumi zaidi ya alichokuwa anakusanya wakala.**

Halmashauri inaomba radhi kwa taarifa za kushtua zilizotolewa na kuomba kutozitia maanani kwani zinaleta taharuki kubwa kwa wananchi na wafanyabiashara wengi na hata kuchafua taswira ya Halmashauri.

Aidha Halmashauri itaendela kuboresha miundombinu mbalimbali kadri itakavyojitokeza ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi wake.



WILLIAM MAGANGA

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI  
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**